



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na. HA.113/388/01/02

Tarehe: 01 April, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi sita (06) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

1.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 06

1.1 MAJUKUMU NA KAZI

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (log book)
- vi. Kufanya usafi wa gari,
- vii. Kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne na Leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali na pia awe na cheti kilichompatia sifa ya kupata madaraja husika. Vilevile awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

TGS B

1.4 MASHARTI YA JUMLA YA MWOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yanayotambuliwa na Mamba ya siku zinazopatikana na

Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/Degree/Advance Diploma/Diploma/Certificates, - Cheti cha Mtihani wa Kidato cha Nne na Sita, Computer Certificate - Vyeti vya Kitaluma (Professional Certificate from Respective Boards).**

- iv. "Testimonial", "Provisional Results", "Statement of Results", hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Kidato cha sita. **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- v. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE)**
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. Waombaji kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika Nafasi za kuingilia waliopo katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika Usahili.
- x. Mwisho wa kutuma maombi ni 12/04/2026
- xi. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa Pamoja na vyeti vya Elimu, Anwani ya barua hiyo ielekezwe kwa;
**Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga,
S.L.P. 28,
SHINYANGA.**
- xii. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia Anuani ifuatavyo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal")
- xiii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na:
